

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

Simu: +255 026 2322761-5
Fax No. +255 026 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz

(Barua zote za kiofisi ziandikwe
kwa **KATIBU WA BUNGE**)

Unapojibu tafadhalii taja:



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Ndugai amemtumia Salamu za Rambirambi Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kufuatia Kifo cha Mke wake Mpendwa Bi Linah George Mwakyembe kilichotokea tarehe 15 Julai 2017 katika Hospitali ya Agha Khan Jijini Dar es Salaam alikokuwa akipatiwa matibabu.

“Mhesimiwa Mwakyembe nakupa pole sana, nimepokea kwa mshtuko na masikitiko makubwa taarifa hii ya kifo cha Mke wako Mpendwa Bi Linah George Mwakyembe , hakika hili ni pigo kwako na kwa familia nzima, namuomba Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.” alisema Mheshimiwa Ndugai.

“Natoa pole kwa Familia, Ndugu, Jamaa na marafiki kwa kupotelewa na mpendwa wenu, Mwenyezi Mungu awape subira, nguvu na faraja katika kipindi hiki kigumu. Wote kwa pamoja tumuombee Mpendwa wetu apumzike kwa Amani” aliongeza Mheshimiwa Ndugai

Imetolewa na:

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano.
Ofisi ya Bunge,
Dodoma

17Julai 2017